**HOTUBA YA KATIBU MKUU KIONGOZI NA MWENYEKITI WA KAMATI TENDAJI YA TNBC KUHUSU UZINDUZI WA VIKUNDI KAZI (VIWANDA, KILIMO, MAZINGIRA YA BIASHARA NA MISITU), IKULU, DAR ES SALAAM, TAREHE 19 NOVEMBA, 2018**

---

***Ndugu Salum Shamte,***
***Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) na***
***Mwenyekiti Mwenza, Kamati Tendaji ya Baraza la Taifa la Biashara;***

***Prof. Faustin Kamuzora,***
***Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera na Uratibu) na***
***Mwenyekiti, Kikundi Kazi cha Mazingira ya Biashara;***

***Prof. Joseph** Buchweishaija,*
***Katibu Mkuu, Wizara ya Viwanda, Biashara na***
***Mwenyekiti, Kikundi Kazi cha Viwanda;***

***Mhandisi** Mathew Mtigumwe,*
***Katibu Mkuu,Wizara ya Kilimo na***
***Mwenyekiti, Kikundi Kazi cha Kilimo;***

***Prof. Adolf Mkenda,***
***Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii na***
***Mwenyekiti, Kikundi Kazi cha Misitu;***

***Wajumbe wote mlioteuliwa kuunda Vikundi Kazi;***

***Wanahabari;***

***Mabibi na Mabwana.***

Napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kujumuika pamoja siku ya leo kwenye shughuli hii ya uzinduzi wa Vikundi Kazi vinne (04) vya Sekta za Viwanda, Kilimo, Misitu na Mazingira ya Biashara vilivyoundwa chini ya Baraza la Taifa la Biashara. Uundwaji wa **Kikundi Kazi kimoja cha Sekta ya Utalii bado unafanyiwa kazi, hivyo uzinduzi wa Kikundi Kazi hicho utafanyika baadae**.

Nachukua nafasi hii kuwashukuru Wajumbe 58 wa Vikundi Kazi mliokwishateuliwa kwa kukubali uteuzi wenu, na kuitikia wito wa kuhudhuria tukio hili la uzinduzi.

Nafahamu kuwa mnayo majukumu mengi katika nafasi zenu, lakini kwamba mmekubali uteuzi huu unaohusu kutekeleza majukumu haya ya ziada, inaonyesha wazi uzalendo wenu pamoja na mapenzi yenu makubwa kwa nchi yetu.

**Nawapongeza na kuwashukuru sana kwa moyo huo wa kuitumikia nchi yetu**.

Aidha, napenda pia nichukue nafasi hii kuwashukuru Wanahabari wote mliohudhuria kwa kufika kwenu kushuhudia uzinduzi huu wa Vikundi Kazi hivi vya Baraza la Taifa la Biashara - TNBC.

**Karibuni sana Wajumbe na Wanahabari wote mliohudhuria.**

**Ndugu Wajumbe na Wanahabari,**

Napenda pia kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Ndugu Salum Shamte kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) baada ya aliyekuwa Mwenyekti wa taasisi hiyo Mzee Reginald Mengi kumaliza muda wake. Nina imani Ndugu Shamte ataendeleza jitihada za kuimarisha ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kupitia nafasi aliyoaminiwa na kupewa na Sekta

Binafsi kuwa Mwenyekiti wao. Hongera sana Bwana Shamte na karibu sana ili tuendeleze pamoja majukumu ya Baraza la Taifa la Biashara.

**Ndugu Wajumbe na Wanahabari**,

Napenda kuwakumbusha kuwa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) liliundwa kwa lengo la kuwa jukwaa la mijadala ya kimkakati kati ya Serikali na Sekta Binafsi (*Public Private Dialogue* – PPD) juu ya masuala yanayohusu uchumi wa nchi yetu. Lengo mahsusi la majadiliano katika jukwaa hili, ni pamoja na kufikia muafaka kuhusu **mwelekeo** wa **shughuli** za uchumi wa nchi yetu, katika **sekta mbalimbali**, sambamba na **kuboresha mazingira** ya kufanya biashara na uwekezaji hapa nchini; na pia kuendeleza juhudi za ukuaji wa sekta binafsi.

Hivyo, Serikali itaendelea kulitumia Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) kama jukwaa la mazungumzo na Sekta Binafsi katika kujadili masuala mbalimbali yenye maslahi mapana kwa Taifa, kwani Serikali inaamini kwa dhati kuwa, ushirikiano na majadiliano kati ya sekta hizi mbili ni muhimu sana kwa ustawi wa uchumi wa Taifa letu. Ni wazi kuwa Baraza la Taifa la Biashara likitekeleza wajibu wake ipasavyo, basi litachangia sana katika kudumisha mazingira ya kuaminiana kati ya Serikali na Sekta Binafasi, kwani Sera, Sheria, Mipango mbalimbali ya Maendeleo ya Jamii na ya Uchumi, na Mipango ya utatuzi wa Changamoto mbalimbali zilizopo itaandaliwa kwa uwazi, na kwa ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

Kwa hiyo napenda kusisitiza kwenu Wajumbe wote mlioteuliwa kuwa, kuundwa kwa Vikundi Kazi hivi vya Baraza la Taifa la Biashara, kuna lengo la kuimarisha na kuboresha zaidi mfumo wa majadiliano uliopo sasa kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, hivyo mnao wajibu wa kuhakikisha kuwa Vikundi Kazi mnavyoshiriki vinakuwa hai, na kutoa mchango utakaofanikisha malengo ya Baraza la Taifa la Biashara kama nilivyokwisha kuyaelezea.

Mtapatiwa hadidu za rejea za ujumla (*Broad TOR*) na mahsusi (*detailed TOR*) ambazo zitaongoza utekelezaji wa majukumu ya vikundi vyenu.

**Ndugu Wajumbe, Mabibi na Mabwana,**

Moja ya vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuishirikisha Sekta Binafsi ipasavyo katika kuendeleza uchumi wa nchi yetu, hivyo Serikali inafanya juhudi za dhati katika kukuza sekta binafsi kwa kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara na uwekezaji hapa nchini. Nia ya Serikali ni kuona kuwa Sekta Binafsi inakua kwa kasi kubwa, ili kujenga uchumi imara na endelevu wa Taifa letu. Itakumbukwa kuwa, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**, alipoingia madarakani mwaka 2015, mara baada ya kukutana na Wabunge, alikutana na Sekta Binafsi na kusisitiza umuhimu wa sekta binafsi katika kujenga **uchumi wa viwanda** nchini.

Katika kufanikisha azma hiyo, Mheshimiwa Rais pia amesisitiza umuhimu wa Baraza la Taifa la Biashara kutumika ipasavyo katika kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali na Sekta Binafsi. Vikundi Kazi vya Baraza la Taifa la Biashara vinavyozinduliwa leo, ni viungo muhimu vya **kukutanisha sekta hizi mbili mara kwa mara,** ili kufanya majadiliano ya kina na kutoa mapendekezo ya mageuzi katika kila sekta husika; na kuboresha mazingira ya biashara na hivyo hatimaye kukuza uchumi wetu.

Vikundi Kazi hivi vinatoa fursa kwa wajumbe mlioteuliwa kutumia uzoefu na ujuzi mlionao kupendekeza maboresho katika maeneo ya sekta husika ili kuleta ufanisi zaidi katika ushirikiano kati ya Serikali na Sekta binafsi.

Hivyo, natoa rai kwenu kwa mara nyingine Wajumbe wote mlioteuliwa kuwa mkatekeleze wajibu wenu kwa **weledi** na **juhudi** kubwa ili kupitia mchango wenu mtakaoutoa, mijadala ya kimkakati kati ya Serikali na Sekta Binafsi ilete ufanisi zaidi kwenye ustawi wa uchumi wa Taifa letu.

**Ndugu Wajumbe na Wanahabari,**

Mtakumbuka kuwa katika Kikao cha 11 cha Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) kilichofanyika tarehe 19 Machi, 2018 chini ya **Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Biashara, Serikali iliahidi kuendelea kutekeleza juhudi za kuondoa changamoto mbalimbali zilizopo, ili kuweka mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara nchini. Kwa muhtasari nitaeleza baadhi ya hatua ambazo Serikali imeshachukua na inaendelea kuzichukua katika kupunguza, na hatimaye kuondoa baadhi ya changamoto hizo.

Napenda kuwafahamisha kuwa Serikali ya Awamu ya Tano inaendelea kufanya maboresho katika maeneo mbalimbali ili **kupunguza gharama za kufanya biashara na uzalishaji**. Hii ni pamoja na kuboresha miundombinu mbalimbali wezeshi iliyo muhimu kama vile barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege, huduma za maji na uzalishaji wa umeme. Pamoja na miradi hii kutoa fursa za biashara kwa Sekta Binafsi ya ndani, ni dhahiri kuwa itakapokamilika itapunguza kwa kiasi kikubwa changamoto za miundombinu ya usafirishaji na upatikanaji wa maji na umeme wa uhakika kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi hapa nchini.

**Ndugu Wajumbe,**

Serikali ya Awamu ya Tano pia inaendelea kuboresha mfumo wa kodi ili uwe wa kisasa zaidi na utakaorahisisha ulipaji kodi, na pia kuwa rafiki kwa walipa kodi. Hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kusisitiza matumizi ya mashine za kieletroniki (EFDs), kuimarisha mfumo wa taarifa za mlipa kodi, na kutoa

elimu ili kuongeza ari ya kulipa kodi kwa hiari (*voluntary compliance*) na kupunguza malalamiko ya walipa kodi.

Aidha, kutokana na Kikao cha 11 cha Baraza la Taifa la Biashara, Serikali imefanya marekebisho ya Sheria mbalimbali kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2018. Sheria zilizorekebishwa ni pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015 ambayo sasa inatoa msamaha maalum wa **riba na adhabu** kwenye malimbikizo ya madeni ya kodi kutoka asilimia 50 ya hapo awali **hadi asilimia mia moja**. Ninawaomba tuendelee kushirikiana kuwahimiza wafanyabiashara wote watumie fursa hii vizuri kwa kulipa malimbikizo yao ya kodi, kwani hawatatozwa **riba** wala **adhabu**.

Serikali pia imeondoa baadhi ya tozo na kero ambazo zimekuwa zikilalamikiwa na Sekta Binafsi, ikiwemo kupunguza ushindani wa bidhaa za Tanzania na bidhaa zinazoagizwa kutoka nje. Hatua zilizochukuliwa na Serikali ili kupunguza ushindani huo katika soko la ndani ni pamoja na:

1. Kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imetoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye usindikaji wa mbegu za mafuta.
2. Serikali imepunguza ushuru wa bidhaa kwenye mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa ndani ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 75 kutoka Shilingi 202 kwa lita kuwa Shilingi 200 kwa lita.
3. Kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imeongeza ushuru wa bidhaa kwa mvinyo unaotengenezwa kwa zabibu zinazozalishwa nje ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 25 kutoka Shilingi 2,349 hadi Shilingi 2,466 kwa lita.
4. Ushuru wa bidhaa kwenye maji ya matunda ikiwa ni pamoja na

zabibu yanayozalishwa hapa nchini umepunguzwa kutoka Shilingi 9.50 hadi Shilingi 9.00 kwa lita.

5. TFDA inakamilisha mapitio ya **Kanuni za ada na tozo** ili kuwa wezeshi zaidi kwa wafanyabishara. TFDA imefuta ada na tozo takriban 25 ili kuwapunguzia gharama wajasiriamali wadogo na wazalishaji wa bidhaa za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba zinazozalishwa ndani ya nchi.
6. Kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali inatoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 kwenye mafuta ghafi ya mawese na alizeti yanayotoka nje ya nchi, pamoja na kuongeza ushuru wa forodha kwenye mafuta ya mawese yaliyochakatwa kwa kiwango cha kati na cha mwisho (*semi-refined and refined palm oil*) kutoka asilimia 25 hadi asilimia 35.

**Ndugu Wajumbe na Wanahabari,**

**Sekta ya Kilimo** bado ina umuhimu mkubwa katika uchumi wa Tanzania. Ni ukweli usiopingika kwamba Sekta ya kilimo bado ndiye mwajiri mkubwa hapa nchini. Sekta hii ambayo inajumuisha wafugaji, wavuvi na wakulima, hasa wale wadogo wadogo, bado inakabiliwa na changamoto nyingi. **Kikundi Kazi cha Kilimo** kinatakiwa kufanya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa nguzo kumi za Kilimo Kwanza, pamoja na kutoa mapendekezo ya utekelezaji wa haraka wa Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo, Awamu ya Pili (ASDP II) na kutoa mapendekezo ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji katika sekta ya kilimo kwa wakulima wadogo na wakubwa.

Vile vile Serikali inaendelea kuimarisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) ili kuhakikisha kwamba inawafikia wakulima wengi zaidi. Mnamo mwaka 2017 Serikali iliipatia Benki hiyo kiasi cha Shilingi bilioni 206 kama mkopo wenye riba nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Benki ya Kilimo imeanzisha utaratibu wa kukopesha kupitia kongani (*Clustering and Value Chain Approach*) ambapo

mikoa yote Tanzania imeunganishwa katika kongani nane (8) zinazoendana na kanda za kiekolojia *(ecological zones*) zinazoainisha mazao ya kipaumbele kwa ajili ya kupatiwa mikopo na benki.

**Aidha, Serikali imeondoa zuio la uuzaji wa mazao ya chakula nje ya nchi,** kwa kufuata utaratibu maalum. Utaratibu huu utapanua soko, na hatimaye kukuza uwekezaji na uzalishaji katika kilimo.

**Ndugu Wajumbe na Wanahabari,**

Serikali inaendelea kuondoa changamoto zinazotokana na taasisi za udhibiti kuhusiana na wawekezaji wa ndani na nje wanaotaka kuwekeza katika **Sekta ya viwanda**. Aidha, taasisi za Serikali zimeanza kushirikiana kwa karibu katika kutoa huduma. Kwa mfano Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linafanya kazi kwa karibu na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) kuhakikisha kuwa wanapunguza kero na vikwazo kwa wafanyabiashara.

TBS na TFDA zimefanya makubaliano ya mashirikiano ili kuleta ufanisi zaidi katika utendaji kazi wao. TBS inapima sampuli za wajasiriamali kwa gharama za Shirika na majibu ya TBS hutambuliwa na TFDA na hivyo hutumiwa na TFDA katika kutoa vibali bila kupima tena.

Kwa sasa TBS imeanzisha Kanda tano ambazo ni Kanda ya Kaskazini, Kusini, Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Ziwa na Kanda ya Kati kwa lengo la kusogeza huduma zake karibu na wazalishaji/wafanyabiashara ili kuwafikia kwa urahisi.

Aidha, Serikali imetoa vivutio kwa Wawekezaji wapya kwenye viwanda vya kutengeneza bidhaa za ngozi na madawa, kwa kupunguza kodi ya makampuni (*corporate tax*) kutoka asilimia 30 hadi 20.

**Ndugu Wajumbe na Wanahabari**,

Napenda pia kuwafahamisha kwamba kuundwa kwa Kikundi Kazi cha Viwanda kumetokana na maombi ya Sekta Binafsi, yaliyowasilishwa kwenye Kikao cha 10 cha Baraza la Taifa la Biashara kuhusu kuunda Kamati ya Viwanda ya Kitaifa, ili kuongeza ushiriki wa Sekta Binafsi kuelekea Tanzania ya Viwanda.

Kikundi Kazi cha Viwanda kinategemewa kutoa mapendekezo yatakayowawezesha watanzania wote na Wawekezaji kutoa nje kushiriki kikamilifu katika kuifikisha nchi yetu katika uchumi imara unaoendeshwa na viwanda.

**Ndugu Wajumbe na Wanahabari,**

Rasilimali za **misitu** ni kichocheo muhimu cha kukuza ajira, uchumi wa viwanda na uhifadhi wa mazingira. Ili kuongeza mchango wa **Sekta ya Misitu** kwenye pato la Taifa, Kikundi Kazi cha Misitu kinapaswa kutafuta **majawabu ya kuwa na uhifadhi na matumizi endelevu ya misitu yetu kuliko ilivyo sasa** na kulishauri ipasavyo Baraza la Taifa la Biashara.

**Ndugu Wajumbe,**

**Mazingira ya Biashara** ni suala mtambuka. Jitihada za maboresho ya mazingira ya biashara kupitia mipango mbalimbali ambayo inatekelezwa na Serikali, ukiwemo Mpango wa *Blueprint for Improvement of Business Licensing and Regulatory Environment,* uliopitishwa na Serikali mwaka huu wa 2018, zinategemewa kupunguza kadhia ya ufanyaji biashara nchini.

**Kikundi Kazi cha Mazingira ya Biashara** kinatakiwa kufanya tathimini na ufuatiliaji wa **Sera**, **Sheria**, **miongozo** na **mipango** yote ya maboresho ya mazingira ya biashara iliyopo kwa lengo la kutoa ushauri na mapendekezo ambayo yataongeza ufanisi na utendaji wa sekta binafsi katika Biashara na Uwekezaji hapa nchini.

**Ndugu Wajumbe**,

Hatua nyingine ambazo Serikali itaendelea kuzichukua katika kuboresha Mazingira ya Biashara nchini ni pamoja na:

(i) Kuimarisha masoko ya mitaji na mfumo wa fedha ili kuhakikisha utulivu wa kiuchumi na ukuaji wa sekta binafsi.

(ii) Kutilia mkazo matumizi ya masoko ya mitaji katika kuhamasisha akiba na uwekezaji katika nchi, na hatimaye kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta binafsi.

(iii) Kuhamasisha Makampuni binafsi kujiorodhesha katika Soko la Hisa Dar es Salaam ili kuwezesha upatikanaji wa mitaji nafuu kwa biashara zilizopo na biashara mpya.

(iv) Kuimarisha udhibiti wa benki za biashara ili kuhakikisha panakuwepo na mfumo imara wa fedha ambao utatenga mikopo kwa sekta zote za uchumi na mikoa yote ili kuhakikisha kuwepo kwa usawa na uwiano wa maendeleo nchini kote.

(v) Kutekeleza mageuzi ambayo yatapanua mfumo wa fedha na kuhakikisha kila Mtanzania anakuwa na urahisi wa kupata huduma za kibenki pamoja na bima, na anatambua faida itokanayo na matumizi ya huduma za kifedha katika kubadilisha na kuboresha maisha ya wananchi.

**Ndugu Wajumbe na Wanahabari,**

Kama nilivyosema hapo awali, Mheshimiwa Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Biashara, anatambua umuhimu wa

kuishirikisha Sekta Binafsi kupitia Majadiliano kati ya Serikali na Sekta Binafsi (PPD) katika kujenga uchumi wa nchi yetu.

Katika juhudi za kuzidi kuimarisha mfumo wa majadiliano kati ya Serikali na Sekta Binafsi, TNBC kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na TPSF wako katika hatua za mwisho kukamilisha **Mwongozo mpya wa Majadiliano** kati ya Serikali na Sekta Binafsi (*PPD Guideline*). Pamoja na mambo mengine, mwongozo huo utaimarisha mfumo wa Mabaraza ya Biashara ya Mikoa na Wilaya ili kuboresha majadiliano kati ya Serikali na Sekta Binafsi katika ngazi ya Mikoa na Wilaya. Mwongozo huo mpya utatolewa hivi karibuni baada ya taratibu zote muhimu zinazopaswa kufanyika kukamilika.

Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru DANIDA kupitia mradi wa *Local Investment Climate (LIC)* pamoja na program ya *Enabling Growth Through Investment and Enterprise (ENGEN),* kwa kufadhili uandaaji wa Mwongozo huo. Aidha, nawashukuru DANIDA kwa kufadhili uendeshaji wa Mabaraza ya Biashara ya Mikoa na Wilaya zote kwa mikoa ya **Dodoma** na **Kigoma**.

Tutaendelea kuwashawishi wadau wengine kuendeleleza juhudi za kuimarisha Mabaraza ya Biashara ya Mikoa na Wilaya ili kuwa na wigo mpana wa majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi hadi ngazi ya Wilaya.

**Ndugu Wajumbe na Wanahabari,**

Nimalizie kwa kuwahakikishia kuwa, michango ya Vikundi Kazi hivi **itathaminiwa ipasavyo na kuzingatiwa**; hivyo narudia tena kusisitiza umuhimu wa Vikundi Kazi vyote kutekeleza majukumu tuliyowapa kwa weledi mkubwa kwa faida ya nchi yetu.

Napenda sasa kuhitimisha kwa kutamka rasmi kuwa **Vikundi Kazi vya Sekta za "Viwanda, Kilimo, Mazingira ya Biashara na Misitu" chini ya Baraza la Taifa la Biashara vimezinduliwa rasmi.**

*Asanteni sana kwa kunisikiliza*